## Mapendekezo

Tungependa kupendekeza yafuatayo:

1. Serikali ilainishe ushuru wa biashara ya uvuvi na utoaji wa leseni kwa njia ya uwazi na uwajibikaji ili kupunguza vikwazo vya urasimishaji na kupunguza hasara za kibiashara. Wauzaji wadogo wadogo washauriwe wakati wa kuratibu ushuru.

2. Twahitajika kuzatiti, kuidhinisha na kuimarisha mauzo pamoja na vyama vya biashara ili kuboresha bei na maduhuli. Tungependa sera zinazotuwezesha na kututia motisha kudhibiti vyama na mitandao.

3. Tungependa ubia ukuzwe kati ya sekta ya umma na ile ya kibinafsi katika mipango ya fedha na mikopo midogo midogo. Mpango huu uzagazwe vijiji vingi vya pwani. Kuimarisha biashara yetu, hatuna budi kupata usaidizi wa kifedha.
4. Ukusanyaji wa ushuru utathminiwe kwa kumithilishwa na mazao ya uvuvi na idadi ya wafanyabiashara katika sekta hii. Ukaguzi wa karibu wa maafisa wa kupambana na ufisadi sharti uwe kanuni.

5. Serikali sharti iimarishe utoaji wa mafunzo juu ya uwekezaji na biashara kwa wauzaji samaki ndani ya mikakati na ari ya kupunguza umaskini nchini.



Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa “uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki” unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC, The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.

Sifa kwa picha: M. Samoilys/IUCN

# Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Tanzania



# Wafanya Biashara ya Samaki na Maendeleo ya Jamii na Uchumi

Na:
Ramadhan H Mwigah
Zainabu Mvaa
Amiri Mkopi
Stella Wissiko

# Utangulizi

Wafanyabiashara wa samaki wapatikana mahali pengi pwani ya Tanzania. Hii ni kutokana na uvuvi wa maji ya kina kifupi uliostawi. Hata hivyo, wafanyabiashara wadogo wadogo wana unyonge wa ujuzi na utaalamu wa biashara na uwekezaji. Hali kadhalika usimamizi wa shughuli zao ni holela.

Warsha ya kitaifa ya jamii ya pwani ilifanyika Tanga kuanzia tarehe 28 hadi 31 Januari 2008. Lengo la warsha lilikuwa kuzipa jamii za pwani fursa ya kutangamana na kubadilishana uzoefu wa usimamizi na utendaji kwenye rasilimali za baharini pamoja na kuelezea kwa ufasaha mahitaji yao. Kama wakilishi wa kikundi cha wafanyabiashara tulitoa maoni yetu, malengo, shughuli, masuala nyeti na mapendekezo katika mkutano huo.



# Wafanyabiashara wa samaki, azma na malengo yao

| JINA LA KIKUNDI | SHABAHA/MANUFAA |
|---|---|
| UMOJA WA WAVUVI WADOGO WADOGO- (UWAWADA)<br>Dar es Salaam | • Kurahisisha ushirikiano baina ya wavuvi, wataalamu wa uvuvi na Wadau wengine kwa minajili ya kuchangia uvuvi bora na uendelevu.<br>• Kuimarisha utawala bora kupitia kampeni za utetezi na mitandao ya habari .<br>• Kuboresha ustawi wa wavuvi wadogo wadogo kupitia ubia kati yao na wadau wa sekta ya uvuvi, ikiwemo serikali<br>• Kuboresha soko na biashara ya wavuvi wadogo wadogo.<br>• Kuhamasisha na kuelimisha wanachama juu ya sera na sheria husika na kuwasilisha mapendekezo kwa halmashauri na serikali kuu. |
| CHAMA CHA USHIRIKA CHA WAVUVI-VUSHA<br>Dar es Salaam | • Kuboresha ustawi, maendeleo na uchumi wa wanachama na jamii kwa kukita mfumo wa kidemokrasia na ushirika.<br>• Kusaidia uvuvi na mauzo ya samaki aina mbalimbali kwa soko la jumla na rejareja.<br>• Kuwasaidia wanachama kupata, miliki na kusimamia vyombo na vifaa vya kisasa vya uvuvi.<br>• Kuwahamasisha na kuwaelimisha wanachama juu ya mfumo wa ushirika. |
| SHIRIKA LA MAENDELEO YA KIUCHUMI LA KIPUMBWI<br>Pangani, Tanga | • Kuendeleza uhifadhi wa mazingira<br>• Kuwawezesha wanachama na jamii kutumia maliasili kwa njia endelevu ili kupunguza umaskini na kustawisha uchumi wao.<br>• Kufanya kilimo cha mwani, uvuvi, ufugaji nyuki na kuzalisha asali, upanzi wa mikoko na wa miti ya barani, ufugaji wa kisasa wa mifugo; na kutoa mikopo midogo midogo. |

# Maswala kipaumbele

Tumetambua yafuatayo kama maswala muhimu yanayoathiri biashara ya samaki:

1. Faida tunayopata kwa biashara ya samaki ni ndogo mno. Kwa sababu tunatozwa ushuru mwingi kiholela kutokana na leseni nyingi zinazohitajika. Hali kadhalika, hapana mpangilio maalum na viwango vya ushuru vinavyowekewa biashara ya samaki.
2. Masomo ya samaki hayategemeki. Bei si imara, hivi basi tunaongezea shida kupanga na kudhibiti biashara. Mara nyingi mfanyabiashara huajibika kutafuta masoko nje na ndani yeye binafsi. Hivyo hutupunguzia uwezo wetu wa kuafikiana bei bora.
3. Mipango na taratibu ya mikopo midogo midogo ya fedha ni michache. Hatuna uwezo wakupata fedha zaidi za kuimarisha biashara yetu.
4. Ukasanyaji wa ushuru umekumbwa na ufisadi. Matokeo yake ni maendeleo duni na ya kudhalilisha katika sekta ya samaki na uvuvi.

